

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA. 14 YA 1990

NAKUBALI,

Rais

5th June 1990

Sheria ya kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweka mfumo mpya wa Tume ya Uchaguzi, utaratibu wa kushughulikia malalamiko ya uchaguzi, na masharti mengineyo

[.....]

SHERIA Hii imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Sita ya Katiba ya Nchi, ya mwaka 1990. Jina la Sheria
2. Ibara ya 74 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo (1) ya ibara hiyo na badala yake kutakuwa na masharti mapya yafuatayo:— Kufuta ibara ndogo ya (1) ibara ya 74 na kuweka mpya
 - (1)(a) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na idadi ya Wajumbe kama itakavyotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge.
 - (b) kazi za Tume ya Uchaguzi zitakuwa kama zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba hii na katika Sheria itakayotungwa na Bunge.
 - (c) Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kusimamia uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha Wilaya za Uchaguzi.
3. Ibara ya 75 ya Katiba inabadilishwa kwa kuongeza chini ya ibara ndogo ya (4) ibara ndogo ifuatayo:— Kurekebis ha Ibara ya 75

"(5) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, hakuna mahakama yoyote itakayokuwa. na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote, lililotendwa na Tume katika utekelezaji wake wa kugawa Wilaya za Uchaguzi.

Kufuta na kuweka ibara ya 83

4. Ibara ya 83 ya Katiba inafutwa. na badala yake kutakuwa na ibara mpya ifuatayo:-

"Uamuzi wa suala kama -mtu ni Mbunge

83.-(1) Bila ya kuathiri ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala kama-

(a) uchaguzi au uteuzi wa, mtu yeyote kuwa Mbunge ulikuwa halali au sivyote; au

(b) Mbunge amekoma kuwa Mbunge na kiti chake katika Bunge ki wazi au hapana,

lalamiko, au malalamiko yanayohusika na suala hilo yatawasilishwa. na kusikilizwa katika Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo.

(2) Iwapo Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 41(3) ya Katiba hii imemtangaza Mbunge yeyote kwamba amechaguliwa kuwa Rais basi hakuna chombo chochote wala mahakama itakayochunguza zaidi suala lolote linalohusu kiti cha Mbunge huyo kuwa wazi.

(3) Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo-

(a) watu wanaoweza kuwasilisha malalamiko katika Tume ya Uchaguzi kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala lolote kwa, mujibu wa masharti ya ibara hii;

(b) sababu na nyakati za kuwasilisha malalamiko kama hayo, utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na masharti-yanayotakiwa yatimizwe kuhusiana na malalamiko kama hayo; na

(c) kutaja mamlaka ya Tume ya Uchaguzi juu ya malalamiko kama hayo na kueleza utaratibu wa kusikiliza na kuamua malalamiko, yenyewe.

(4) Uamuzi wa Tume ya Uchaguzi juu ya lalamiko lolote lililosikilizwa na Tume kwa mujibu wa ibara hii utakuwa ni wa mwisho na hautahojwa, katika mahakama au chombo kingine chochote katika Jamhuri ya Muungano

Kurekebisha ibara ya 109


5. Ibara ya 109 inarekebishwa--

(a) Katika ibara ndogo ya (2), kwa kufuta maneno "Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufani Tanzania aliyetajwa katika ibara ya 118 ya Katiba hii" yanayoonekana katika mstari wa pili na wa tatu, na badala yake kuweka maneno "Tume ya Kuajiri ya Mahakama";

- (b) Katika ibara ndogo ya (3), kwa kufuta maneno “ibara ndogo ya (2) ya ibara hii” na badala yake kuweka maneno “ibara ya 118”;
- (c) katika ibara ndogo ya (9), kwa kufuta maneno “Jaji Mkuu kama kawaida” na kuweka badala yake maneno “Tume ya Kuajiri ya Mahakama”.
6. Ibara ya 112 inarekebishwa kwenye ibara ndogo ya (1)—
- (a) kwa kuweka baada ya aya (a) aya ifuatayo:—
 “(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali,”;
- (b) kwa kubadili aya (b), (c), na (d) kuwa aya (c), (d) na (e).

Kurekebis
ha Ibara
ya 112

Passed in the National Assembly on the eleventh day of April, 1990.



M. Mwinuka
Clerk of the National Assembly